



OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA IRINGA



Barua zote ziandikwe kwa:
Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya
Simu nambari +255 (026) 2701776//27020580/2701775
Nukushi +255 (026) - 2702828

S.L.P.108
IRINGA,
TANZANIA

Baruapepe:ded@iringadc.go.tz

Kumb.Na. IDC/S.20/III/87

26/06/2023

TANGAZO LA NAFASI YA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Iringa anakaribisha maombi ya kazi kwa wataanzania wote wenye sifa na uwezo wa kujaza nafasi ya **MSAIDIZI WA KUMBUKUMBU DARAJA LA II**. Tangazo hili ni kutokana na kibali cha ajira Mbadala chenye Kumb. Na. FA.170/363/01"A"/81 cha tarehe 31/05/2023 kutoka kwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala bora. Nafasi hizo za kazi ni zifuatazo:

1.0 MSAIDIZI WA KUMBUKUMBU DARAJA LA II NAFASI (1)

1.1 SIFA ZA MWOMBAJI:

- Awe amehitimu Elimu ya kidato cha nne au sita wenye stahhahada (NTA Level 6) katika fani ya urasimu ramani (Cartography) au (geoinformatics) sheria, Afya, au Masjala kutoka vyuo vinavyotambuliwa na serikali, wenye ujuzi wa kompyuta.

2.1 MAJUKUMU YAKE:

- Kuorodhesha barua zinazolingia masjala kwenye regista (incoming correspondence register)
- Kuorodhesha barua zinazotoka nje ya taasisi (outgoing correspondence register)
- Kusambaza majalada kwa watendaji (action officers)
- Kupokea majalada yanayorudi masijala toka kwa watendaji
- Kutafuta kumbukumbu/nyaraka/majalada yanayohitajika na watendaji
- Kurudisha majalada kwenye shubaka/kabati la majalada (racks/filling cabinets) au mahalipengine yanapohifadhiwa
- Kufuatilia mzunguko wa majalada ndani ya taasisi (file tracking)

NGAZI YA MSHAHARA TGS C

MASHARTI YA JUMLA KWA WAOMBAJI WA KAZI ZOTE.

- i. Mwombaji awe ni Raia wa Tanzania
- ii. Awe na umri usiopungua miaka 18 na usiozidi miaka miaka 45.
- iii. Maombi yote yaambatishwe na nakala ya cheti cha Taaluma, cheti cha Kidato cha Nne, cheti cha kuzaliwa na kitambulisho cha uraia au namba ya NIDA.
- iv. Maelezo binafsi yanayojitosheleza (CV) ikiwa na anuani, namba za simu za kuaminika, majina matatu ya wadhamini na picha mbili (Passport Size) za hivi karibuni.
- v. Vyeti vyote vya Taaluma, Kidato cha Nne na cheti cha kuzaliwa vithibitishwe na Hakimu/Wakili anayetambulika na Serikali.
- vi. Aidha, uwasilishaji wa taarifa na sifa za kugushi wahusika watachukuliwa hatua za Kisheria na Mamlaka zinazohusika.
- vii. Watumishi waliopunguzwa kazi/kufukuzwa kazi Serikalini hawaruhusiwi kuomba.
- viii. Testimonials, results statement of results na hati za matokeo ya Kidato cha Nne/Sita (Form IV na Form VI result slip) havitakubalika.
- ix. Mwombaji yeyote ambaye hatazingatia mojawapo ya masharti au vigezo tajwa hapo juu maombi yake hayatahughulikiwa.
- x. Kumbuka kuambatisha barua yako ya maombi ya kazi iliyosainiwa iliyoandikwa kwa Kiswahili au Kiingereza na barua hiyo ielekezwe kwa:-




**Mkurugenzi Mtendaji (W),
Halmashauri ya Wilaya ya Iringa,
S.L.P. 108,
IRINGA.**

**MKURUGENZI MTENDAJI (W)
HALMASHAURI YA WILAYA
IRINGA**

Mwisho wa kupokea maombi ya kazi ni tarehe **09 Julai, 2023** saa **09:30 Alasiri**.

Imetolewa na:



**Bashi P. Muhoja
MKURUGENZI MTENDAJI (W)
IRINGA.**

**MKURUGENZI MTENDAJI (W)
HALMASHAURI YA WILAYA
IRINGA**

Nakala: Mbao za Matangazo

: Tovuti ya Halmashauri